


Jinsi ya kupata mavuno mengi kutoka kwa mbegu inayovumilia ukame

Kabla ya kupanda



1

Ikiwezekana, baada ya kuvuna wacha mabaki ya mimea shambani. Hii ni mhimu kwa sababu itasaidia kurejesha, kuhifadhi na kuongeza rutuba mchangani siku zijazo.



2

Tunakushauri utafute mawaidha zaidi kuhusu kilimo cha CONSERVATION AGRICULTURE. Hii itakusaidia kupunguza gharama ya utayarishaji wa shamba.



3

Kabiliana na magugu kabla hayajatoa mbegu kabla na baada ya kuvuna mahindi. Hii ni muhimu kwa sababu itapunguza athari ya magugu shambani mwako misimu ijayo.



4

Kabla ya kununua mbegu, tafuta ushauri wa wataalamu wa kilimo kuusu kiwango cha mbegu unachofaa kupanda. Hii itakusaidia kununua kiwango kinachostahili.



5

Tafadhalii hakikisha unanunua mbegu za kustahimili ukame kutoka kwa muuzaji ambaye amejlandikisha na anafahamika.



6

Pata maelezo kuhusu mbolea mwafaka, kiwango kinachofaa na wakati unaofaa kuitumia kutoka kwa wataalamu wa kilimo wenye uzoefu.




USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

CIMMYT^{MR}
International Maize and Wheat Improvement Center

Jinsi ya kupata mavuno mengi kutoka kwa mbegu inayovumilia ukame


Nafasi za kupanda



Unashauriwa kupanda mbegu moja ya mahindi yanayostahimili ukame katika kila shimo.

Umbali kati ya shimo hadi shimo iwe ni **sm 30**, na umbali kati ya mstari na mstari iwe ni **sm 75**.

Mashimo yawe na kina cha sm 3–5



Kama utapanda kabla ya mvua mashimo yasipungue kina cha sm 5 kuzuia uotaji wa mvua nyepesi



Mbolea ya kupandia iwekwe sm 2.5–5 chini pembedi ya mbegu na isigusane na mbegu



Weka mbolea ya kukuzia mahindi yakiwa na wastani wa majani sita



Palizi ya kwanza ifanyike kabla ya siku 28 tangu mahindi kupanda.



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

CIMMYT^{MR}
International Maize and Wheat Improvement Center

Aina ya mbegu ya mahindi yanayostahimili ukame, au Drought Tolerant (DT) Maize kwa Kiingereza, yanapatikana sasa. Kuwepo kwa aina hii ya mahindi kumetokana na utafiti wa zaidi ya miaka kumi, ukiongozwa na shirika la kimataifa la utafiti, CIMMYT, na kusambazwa na washiriki wake wa kilimo nchini mbalimbali mashariki, magharibi, na kusini mwa Africa.